WIKI YA ASASI ZA KIRAIA 2018

Tarehe: 22-26 Oktoba 2018
Mahali: Dodoma, Tanzania

MWONGOZO KWA WASHIRIKI WA MAONESHO

KAULIMBIU: TANZANIA YA VIWANDA: WATU, SERA NA UTEKELEZAJI

A: UTANGULIZI

Wiki ya Asasi za Kiraia ni fursa adhimu kwa Asasi kujumika na wananchi pamoja na wadau wa maendeleo ikiwemo taasisi za serikali na Bunge ili kutimiza malengo ya Asasi washiriki pamoja na malengo ya Sekta ya Asasi za kiraia nchini. Wiki hii itaambatana na maonesho ya kazi za Asasi, warsha, makongamano pamoja na mijadala.

Madhumuni ya Maonesho:-

- Kuonesha Umma wa Watanzania kazi na huduma zinazotolewa na Asasi za Kiraia
- Kueleza mafanikio na mchango wa Asasi katika maendeleo ya sekta mbalimbali hapa nchini
- Kuimarisha mahusiano na ushirikiano miongoni mwa Asasi, pamoja na wadau muhimu wa maendeleo
- Kuhabarisha Umma kuhusu masuala mbalimbali yanayoshughulikiwa na Asasi za Kiraia
- Kutoa huduma mbalimbali kwa wakazi wa Dodoma ikiwemo upimaji wa afya, ushauri nasaha, ushauri wa kisheria n.k

B: WALENGWA

Maonesho haya ni fursa ya kipekee kwa Asasi kukutana na wadau mbalimbali kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujifunza.

Walengwa wa Maonesho haya ni pamoja na;

- Mawaziri, Maafisa wa serikali kutoka wizara, idara na wakala mbalimbali
- Wabunge
- Asasi za Kiraia
- Wananchi
- Wanafunzi kutoka vyuo vikuu, shule za sekondari na za msingi
- Wafanya biashara na wajasiliamali
- Wanazuoni
- n.k

C: LUGHA

Lugha zitakazotumika ni Kiswahili na Kiingereza. Hii itasaidia wananchi wengi kushiriki kikamilifu na kuelewa maudhui ya wiki hii na kazi za asasi kwa ufasaha zaidi.

D: NAMNA YA KUFANYA MAONESHO

AZAKI zinazokusudia kushiriki katika Maonesho zinatakiwa kuonesha ubunifu katika uwasilishaji wa kazi zao. Aidha maonesho yanapaswa kufanyika kwa ubora wa kiwango cha juu ili kuvutia wadau na wageni wa ngazi zote.
Zifuatazo ni njia mbalimbali zinazopendekezwa kutumika katika kufanya Maonesho:

- Picha na vielelezo – picha, ramani na michoro zinaweza kutumika.
- Vifaa vya sauti - matumizi ya picha zinazoongea, simulizi zilizo rekodiwa pamoja na muziki
- Makala – Kwa njia ya filamu, kanda za video, CD n.k
- Vifaa vya teknologia ya habari – programu mahsusi zilizo kwenye kompyuta, vifaa vinavyotumia sauti na picha
- Mabango – yenye picha au maandishi
- Vielelezo - Vyenye picha, michoro au maandishi
- Maelezo kwa njia ya nyimbo, maigizo, mashairi moja kwa moja kutoka kwa waoneshaji
- Machapisho- vipeperushi, majarida na maandiko mbalimbali,
- Utoaji wa huduma kwa wananchi – Ushauri wa kisheria, nasaha, upimaji wa afya kama vile macho, presha (BP), VVU na kansa
- Na vingine vingi

E: MWONGOZO WA UWASILISHAJI

Washiriki wapaswa kuzingatia yafuatayo katika uwasilishaji : Kutoa utambulisho wa Asasi na shughuli zake, eneo Asasi inapofanyia kazi, miradi na huduma, mafanikio na mchango wa Asasi katika maendeleo ya nchi. Aidha, maelezo na uwasilishaji ujikite katika kaulimbiu **Tanzania ya Viwanda: Watu, Sera na Utekelezaji.**

Izingatiwe kuwa wageni watakuwa na muda mfupi wa kutembelea mabanda ya maonesho. Hivyo basi, Asasi zinapaswa Kufanya mawasilisho yao kwa ufupi na ufasaha. Vitu vitakavyoonyeshwa lazima viwekwe alama.

F: MPANGILIO

Sehemu ya Maonesho itakuwa wazi kuanzia Jumapili Oktoba 21 hadi Jumamosi ya Oktoba 27. Kamati ya Maandalizi itatoa vibanda vya Maonesho kwa mpangilio wa mikoa na kanda ili kurahisisha matumizi bora ya nafasi iliyopo. Mpangilio huu pia utawezesha wageni wakiwemo wabunge, kutambua kwa urahisi Asasi zilizopo katika majimbo na mikoa yao.

G: VIFAA VYA MAONESHO

Waandaaji wa Maonesho watatoa mahema, mabanda (3mx3m), meza moja ndefu, viti viwili, nyanya za umeme na mabango ya kuzitambulisha Asasi zinazofanya maonesho.

Aidha Asasi zitajitegemea kwa mahitaji ya ziada ya maonesho. Asasi ziwasiliane na kamati ya maandalizi mapema ili kupatiwa vifaa hivyo. Gharama za nyongeza zitahitajika.

H: UTARATIBU WA KUJISAJILI

Ili kupata sehemu ya kufanya maonesho, tafadhali jaza fomu ya usajili iliyoambatanishwa au angalia kwenye tovuti ya www.thefoundation.or.tz. Maelezo ya ziada kuhusu Asasi zitakazoshiriki maonesho, pamoja na mada mbalimbali za maonesho yatatolewa. Asasi na mitandao ya mashinani zitapewa kipaumbele.

Maombi kwa ajili ya kufanya maonesho sharti yafanywe kupitia fomu iliyoambatanishwa katika mwongozo huu.

Ushiriki wako katika maonesho utatokana na uchangiaji gharama ya **Shilingi laki tatu (Shilingi 300,000/)** kwa siku zote tano za maonesho, fedha hizi zitumwe kupitia akaunti ya benki iliyotolewa ifikapo **tarehe 05 Oktoba, 2018.** Taasisi au Asasi haitaweza kushiriki maonesho bila kukamilisha malipo haya. Malipo yatatumika kufanikisha upatikanaji wa mahitaji ya maonesho kama mahema, viti, meza, umeme, ulinzi n.k. Ili kuhakikisha asasi nyingi zinashiriki katika maonesho haya, Asasi zinaweza kuungana na kutumia banda moja kama njia ya kupunguza gharama za kushiriki katika maonesho.

Tafadhali wasilisha Fomu ya usajili iliyokamilika kabla ya Tarehe 05 Oktoba, 2018.
Kwa mawasiliano zaidi: Barua Pepe: csoweek2018@thefoundation-tz.org / Tovuti: www.thefoundation.or.tz
Simu / WhatsApp: +255 762 767 237 / Instagram: csoweek2018 / Twitter: @FCSTZ / Facebook: FCSTZ